

meet your RENTON NEIGHBOR


KUTANA NA **Miny Tafesse ›**

- ✿ **MSUKUMO WA NGUVU CHANYA**
- ✉ **MMILIKI WA, SALUNI NA KITUO CHA UREMBO CHA ABYSSINIA**
- 📅 **MIAKA YA KUWA KULE RENTON: 6**

Familia ya Miny Tafesseilimtaka awe mwanasheria. Badala yake, alifuatilia shauku yake ya tasnia ya urembo na sasa anamiliki vituo vitatu vya Kliniki ya Urembo ya Abyssinia.

Alifungua saluni yake ya kwanza ya Abyssinia mwaka wa 2000 jijini Nairobi, Kenya, ambako alikulia. Alihamia Kaskazini Magharibi mwa Pasifikasi ili awe karibu na ndugu yake mdogo. Huku akitafuta mahali pa kufungua saluni, alipata kule Renton.

- ▼ *Miny Tafesse ana vifaa vya kazi vya kuwasaidia wateja kupata mwonekano ulio sahihi pale kwenye Kliniki ya Nywele na Urembo ya Abyssinia mjini Renton.*



- ▲ *Miny Tafesse huwasalimia kwa furaha wateja wa Saluni na Kliniki ya Urembo ya Abyssinia kule Renton. Alifungua saluni yake ya kwanza nchini Kenya mwaka wa 2000.*

UkarimuwaMiny, ujuzi wake wa mitindo na maono ya kibashara yaameifanya Abyssinia kufauli kule Renton tangu saluni hiyo kufunguliwa mwaka wa 2014.

Kisha COVID-19 ikazuka.

“Janga hili lilinitikisa kwa wiki chache,” alisema. Saluni hiyo ilibidi kufunga biashara, na Abyssinia ilikalewesha mipango ya upanuzi wa biashara.

Jamii ilikuja pamoja, mmiliki wa nyumba yake ya biashara alikuwa mwepesi kuelewa hali na mnamo tarehe 6 Juni waliruhusiwa kufungua upya pamoja na kuzingatia hatua za kiusalama.

- ▼ *Abyssinia huzingatia mwongozo wa kiusalama wa COVID-19 kwa ajili ya wateja na wahudumu.*



"Pindi tu nilipogeza kibao cha kuashiria biashara 'imefunguliwa' tulipata wateja kwa wingi," Miny alisema.

Tangu wakati huo amekuwa akifungua mapema na kufunga akiwa amechelewa ili kushughulikia wateja huku akizingatia mwongozo wa jimbo' wa uendeshaji biashara.

"Ukifanya kazi kwa bidii, biashara yako itainuka tena," alisema. "Ukiwa na nguvu chanya, utafanikiwa."

Miny anapanga kutumia nguvu chanya ili kutoa mafunzo kwa watu wengi na kufungua vituo zaidi, na kuwasaidia wanamitindo wa urembo kupanua biashara zao.

Kule kukutana na watu tofauti tofauti ni furaha ya tasnia hii, Miny alisema. Haswa, ye ye hupenda kuwa mionganoni mwa watu wa Marekani wa asili za mataifa mbalimbali

Asili yake ya Kiafrika kamwe haijawahi kuwa kikwazo wakati anapohusika na ye yote mjini.

"Hakuna mtu aliyenichukua kwa namna tofauti au kunitilia shaka. Swal tu la pekee watu huuliza ni iwapo nina muda wa ku wahudumia leo!"❖

Ukianya kazi kwa bidii... utafanikiwa."

✓ Kupaka nywele rangi ni mojawapo ya huduma kuu pale Abyssinia. Saluni ya pale Renton huhudumia wanawake, wanaume na watoto.



▲ Mashauriano yapo ili kuwasaidia wateja kupata bidhaa sahihi za nywele kwa ajili ya mahitaji yao.



▲ Wanamitindo hutengeneza mazingira yasiyo na msongo wa kimawazo, na ya utulivu kwa wateja katika Kliniki ya Nywele na Urembo ya Abyssinia.



▲ Abyssinia iliingia Renton mwaka wa 2014. Mmiliki wake, Miny Tafesse alifungua saluni yake ya kwanza nchini Kenya mwaka wa 2000.